

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA ELIMU YA AWALI DARAJA LA A**

684


VITENDO VYA KUJIFUNZA SANAA

Muda: Saa 3

Mwaka: 2020

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu B na C.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Kwa kutumia michoro, tofautisha kati ya picha njiti na bapa.
2. Taja vifaa viwili unavyoweza kuvitumia kuwasilisha dhana ya rangi kwa watoto wa Elimu ya Awali na kwa kila kimoja elezea jinsi utakavyokitumia.
3. Elezea kwa kifupi hatua nne za usanii wa picha kwa rangi za maji.
4. Kwa kifupi, eleza umuhimu wa unamu mwororo na kwaruzi. Toa hoja mbili kwa kila unamu.
5. (a) Eleza maana ya kuchapa.
(b) Bainisha hatua tatu za kuchapa sarafu ya Shilingi Mia Mbili kwa njia ya kusugua.
6. Ainisha sifa nne za zana za kufundishia na kujifunzia somo la Vitendo vya Sanaa.
7. Taja hatua nne za utengenezaji wa yai kwa kutumia udongo wa mfinyanzi.
8. Bainisha mbinu nne zinazofaa kufundishia mada ya ufinyanzi kwa watoto wa Elimu ya Awali.
9. Ukiwa ni mwalimu wa somo la Vitendo vya Sanaa mtarajiwa, taja misingi minne ya kuzingatia katika uundaji wa vifani mbalimbali.
10. (a) Eleza maana ya wimbo.
(b) Bainisha hatua tatu za kufundisha wimbo mpya kwa watoto wa Elimu ya Awali.

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. Chambua vifaa sita vya uchoraji vinavyotumiwa na watoto wa Elimu ya Awali na kila kimoja eleza sifa yake.
12. Kwa kutumia mifano, fafania manufaa sita anayopata mtoto wa Elimu ya Awali anaposhiriki katika uundaji wa vifani mbalimbali.
13. Kwa kutumia michoro, eleza hatua sita za utengenezaji wa kifani cha ngoma sahili.

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

14. Chambua vigezo sita ambavyo mwalimu anapaswa kuvizingatia anapochagua mbinu za kufundishia Vitendo vya Sanaa kwa watoto wa Elimu ya Awali.
15. Kwa kutumia mifano ya umahiri wa *Upakaji Rangi*, eleza vipengele vifuatavyo vya Andalio la Somo:
 - (a) Umahiri mkuu
 - (b) Umahiri mahususi
 - (c) Shughuli za kutendwa na mwalimu
 - (d) Shughuli za kutendwa na mtoto
 - (e) Viashiria pendekezwa vya utendaji
16. Chambua mambo matano muhimu ambayo mwalimu wa Elimu ya Awali anapaswa kuyaandaa kabla ya kufundisha.